## Maswali

1. Mbona Mungu hakutaka watu wachukue kitu chochote kutoka Yeriko?
2. Wapelelezi walisema nini juu ya Ai?
3. Wanaume wangapi walienda kupigana na Ai?
4. Nini ilifanyika walipopigana na Ai?
5. Mbona Mungu hakuwasaidia?
6. Nani alitenda dhambi? Alifanya nini? Aliadhibiwa namna gani?
7. Tunajifunza nini kutoka kwa Akani?
8. Yoshua aliambia watu 30,000 wafanye nini?
9. Wanajeshi wa Israeli wengine walifanya nini? Ai ilishindwa namna gani?
10. Nani aliambia Yoshua vile anaweza kushinda Ai?

## Majibu

1. Mungu alikuwa ameshinda Yeriko. Hazina ilikuwa ni ya Mungu
2. Ai haina watu wengi wakupigana. Itakuwa rahisi kushinda.
3. Watu 3,000 tu walienda kupigana na Ai.
4. Watu 36 waliuwawa. Waisraeli walitoroka. Walishindwa.
5. Mungu hakuwasaidia kwa sababu mmoja wao alikuwa amekaidi na kutenda dhambi.
6. Akani. Alikuwa ameiba dhahabu, fedha na joho kutoka Yeriko. Akani na kila chochote chake kiliharibiwa
7. Lazima tufanye yenye Mungu ameamrisha tufanye.
8. Yoshua aliambia watu 30,000 waende Ai usiku na wajifiche nyuma ya Ai.
9. Kesho yake, jeshi la Israeli lilienda kushambulia Ai. Walindanganya wanatoroka . Watu wa Ai waliwafuata. Waliojificha walitoka na kuharibu mji. Jeshi la Ai lilinaswa na kuuwawa.
10. Mungu aliambia Yoshua vile anaweza kushinda Ai.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2 Mwaka wa 1

# 30 Waisraeli wanashinda Ai

**Kwa Biblia** Yoshua mlango wa 7 na mlango wa 8:1-26

## Kiini cha somo

Kuonyesha vile ni la maana kutii amri za Mungu kabisa.

## Somo

Wakati jeshi lilishinda mji, askari walikubaliwa kuchukua kila kitu kwa huo mji. Hazina ilikuwa ya watu walioshinda. Waisraeli waliposhinda Yeriko, ni Mungu ndie aliwapa ushindi. Kwa hivyo hazina hiyo ilikuwa ya Mungu. Mungu aliamrisha Waisraeli waweke dhahabu na fedha yote waliyopata Yeriko ndani ya hazina ya Mungu. Lazima wasijiwekee kitu chochote kutoka Yeriko.

Kulikuwa na mji mdogo kwa vilima karibu na Yeriko. Mji uliitwa Ai. Mji wa Ai haukukuwa mbali na barabara ya kwenda Kanaani. Ilikuwa vizuri Waisraeli wachukuwe Ai pia.

Yoshua alituma wapelelezi wachunguze Ai. Wapelelezi walikuja na habari nzuri. Ai haikukuwa na watu wakupigana. Waisraeli wangeshinda kwa urahisi. Barabara ya kuenda Ai ilikuwa mita 1,000, na ni ya mlima. Ilikuwa shida kupanda. Yoshua aliamua kwamba watu elfu tatu tu, wataenda kupigana na watu wa Ai kutoka kwa jeshi lake. Wanajeshi wengine wangebaki na wapumzike.

Wale watu elfu tatu wakapanda juu mlimani. Walienda kupigana na watu wa Ai. Walikuwa na uhakika kwamba watashinda na kuchukuwa mji wa Ai. Mfalme wa Ai na jeshi lake walikuja kukutana na Waisraeli. Waisraeli 36 waliuwawa na jeshi lao likashindwa na watu wa Ai.

Waisraeli waliteremka kwa mlima wakitoroka. Walirudi kwa kambi ya Israeli. Waliambia Waisraeli kwamba mfalme wa Ai na jeshi lake wamewashinda. Yoshua na Waisraeli waliogopa na kuwa na wasiwasi sana. Mungu hakukuwa amewasaidia kushinda watu wa Ai. Makosa ilikuwa wapi?

Yoshua aliomba Mungu. Mungu alimwambia kwamba Mwisraeli mmoja alikuwa amefanya dhambi. Kuna mtu ameiba hazina ya Mungu waliyopata kutoka Yeriko. Mungu alikuwa amewaamru kwamba mtu yeyote asichukuwe kitu kutoka kwa vitu vya Yeriko. Mungu hakusaidia Waisraeli kwa vita vya Ai kwa sababu kuna mtu aliyekaidi amri. Lakini Yoshua hakujua huyu mtu wala hakujua aliiba nini.

Asubuhi iliyofuata, Yoshua alisanya Waisraeli wote pamoja. Aliwambia kwamba Mungu atawaonyesha mtu aliyetenda dhambi. Makabila kumi na mbili ya Israeli walikuja mbele ya Yoshua. Mungu alimwambia achukuwe kabila ya Yuda. Jamii ya Yuda walikuja mbele ya Yoshua. Jamii ya Wazera ikachakuliwa.

Wazera walikuja mbele ya Yoshua mmoja mmoja. Zabdi alichakuliwa. Zabdi alileta jamii yake mmoja mmoja mbele ya Yoshua. Akani alichakuliwa. Mungu alionyesha Yoshua mtu aliyetenda dhambi –alikuwa Akani.

Yoshua aliambia Akani atubu hiyo dhambi. Akani alitubu. “Utapata hazina niliyoiba kutoka Yeriko imezikwa chini ya hema yangu. Niliiba joho maridadi, kipande cha dhahabu na fedha kadhaa.” Mungu alimwambia Yoshua aangamize Akani na kila kitu chake kwa sababu alikuwa amekaidi Mungu.

Mungu alimwambia Yoshua kwamba atasaidia Waisraeli washinde Ai. Mungu alipea Yoshua maagizo. Mungu aliambia Yoshua nini yenye lazima Waisraeli wafanye.

Mungu aliambia Yoshua kwamba ifikapo usiku atume watu elfu thelathini wajifiche upande mwingine wa Ai. Hawa watu walikuwa mafichoni ili wawafumanie watu wa Ai. Wanajeshi waliosalia walienda wazi kushambulia Ai. Baadaye walijifanya kama wanatoroka kutoka kwa jeshi la Ai na mfalme wao. Wakati watu wa Ai walitokea kuwafauta, waliokuwa mafichoni walitoka na kushambulia mji.

Yoshua alituma watu elfu thelathini. Walienda usiku mpaka upande mwingine wa mji wa Ai na wakajificha. Ilipofika asubuhi, Yoshua aliongoza wanajeshi wengine mpaka Ai. Mfalme wa Ai na jeshi lake walitoka kupigana nao. Waisraeli walitoroka vile walivyofanya mara ya kwanza. Wanajeshi wa Ai waliwafukuza.

Watu wa Ai wote walitoka mjini mbio na kufukuza Waisraeli. Halafu Yoshua aliinua mkuki. Hii ilikuwa ishara kwa waliokuwa mafichoni upande mwingine wa Ai. Waliokuwa mafichoni walitoka. Hakukuwa na wanaume waliosalia mjini kuwapinga. Waisraeli waliokuwa mafichoni walishambulia mji, wakaiharibu na kuichoma.




Wanaume wa Ai waliona mji wao unaungua. Waisraeli waliaacha kutoroka. Waligeuka kupigana na jeshi la Ai. Waisraeli waliokuwa mafichoni walitokea nyuma ya mji na kushambulia jeshi la Ai. Jeshi la Ai lilinaswa katikati ya Waisraeli. Waliuwawa wote.




Yoshua alitengeneza madhabahu. Waisraeli wote walitoa dhabihu ya kumhimidi Mungu. Walishukuru Mungu kwa kuwasaidia kushinda Ai.